
# UZALISHAJI BORA WA MBUZI WA NYAMA

## mtunze mbuzi akutunze



NA

EDITH E. NDEMANISHO

# UZALISHAJI BORA WA MBUZI WA NYAMA

## mtunze mbuzi akutunze

NA

EDITH E. NDEMANISHO

YALIYOMO

UTANGULIZI ........................................ 1
SURA YA KWANZA ........................................ 1
HALI YA SASA YA UFUGAJI WA MBUZI TANZANIA ........................................ 1
SURA YA PILI ........................................ 4
UZALISHAJI ........................................ 4
Malengo katika uzalishaji wa mbuzi wa nyama ........................................ 7
SURA YA TATU ........................................ 9
ULISHAJI ........................................ 9
SURA YA NNE ........................................ 12
AFYA YA MBUZI ........................................ 12
SURA YA TANO ........................................ 19
MABANDA ........................................ 19
SURA YA SITA ........................................ 21
UTUNZAJI KUMBUKUMBU ........................................ 21

# UTANGULIZI

Kitabu hiki cha "Uzalishaji Bora wa mbuzi wa Nyama" kimetayarishwa na mtaalam na mfundishaji wa somo la mbuzi na kondoo kwenye Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kwa zaidi ya miaka 35, Profesa Edith Ndemanisho. Lengo kubwa la kitabu hiki ni kuwaelimisha wafugaji wadogo wadogo wa mbuzi juu ya ufugaji wa kisasa ili kuongeza pato na lishe kwa familia. Aidha, kimetayarishwa kwa kutumia lugha rahisi inayomwezesha mkulima kuelewa yaliyomo kwa urahisi. Nchini Tanzania kuna mbuzi wanaokadiriwa kufikia milioni 24.5. Hadi sasa, kuna miradi michache ya utafiti na maendeleo ya uzalishaji wa wanyama hawa. Wafugaji wa mbuzi hawajaelimishwa juu ya mbinu mbali mbali za uzalishaji. Kwa hiyo kuna matatizo mengi yanayoathiri shughuli za uzalishaji wa mbuzi ikiwa ni pamoja na ulishaji bora, uzalishaji (breeding), mabanda, magonjwa na utunzaji kwa ujumla. Soko la mbuzi ni kubwa hasa katika nchi za Uarabuni na huwa wanatafuta mbuzi wa nyama kwa wingi kutoka Tanzania. Ni vyema wafugaji wa mbuzi wakachangamkia hili soko kwani majirani zetu Kenya huwa wanao mbuzi bora ila idadi yake sio kubwa kama ya nchini Tanzania.

Mbuzi wa nyama wanaweza kufugwa kwa gharama nafuu, kuishi katika mazingira magumu kama ya maradhi na ukame ikilinganishwa na ng'ombe. Kutokana na umbile lao dogo wanaweza kufugwa katika eneo dogo na pia wanaweza kuhudumiwa na familia (hata wanawake na watoto) yenye nguvu kazi na kipato kidogo. Uzao wao ni wa muda mfupi (wanabeba mimba kwa miezi mitano tu) unamwezesha mfugaji kupata mbuzi wengi kwa kipindi kifupi. Wanyama hao hufugwa kwa ajili ya nyama, maziwa, ajira, ngozi, mbolea, manyoa (Fleece na Cashmere) na mazao mengine kwa matumizi ya familia na kuongeza kipato.

Kitabu hiki kinaeleza mbinu mbali mbali juu ya utunzaji bora wa mbuzi na kimegawanywa katika sura kuu sita ambazo ni *Hali ya sasa ya ufugaji wa mbuzi Tanzania*, *uzalishaji*, *ulishaji*, *afya ya mbuzi*, *mabanda* na *utunzaji kumbukumbu*.

## SURA YA KWANZA

## HALI YA SASA YA UFUGAJI WA MBUZI TANZANIA

**Kwa nini mbuzi?**

Mbuzi ni wanyama wadogo ambao wakulima wenye kipato kidogo wanaweza kuwapata na kuwatunza kwa urahisi ukilinganisha na wanyama wakubwa kama ng'ombe. Mbuzi wana faida zifuatazo:

- Wanachangia kipato cha mkulima kutokana na mauzo ya wanyama hai.

- Wanaweza kuzaa mapacha hadi wanne kwa mzao mmoja na hivyo huongezeka kwa haraka
- Wanahitaji sehemu ndogo ya malisho ikilinganishwa na wanyama wakubwa.
- Samadi yao inaweza kutumika kuongeza uzalishaji wa mazao kama mbolea badala ya mbolea za viwandani.
- Mtaji mdogo unahitajika kuanza mradi wa uzalishaji wa mbuzi
- Mbuzi wana nafasi maalum katika jamii. Kwa mfano, baadhi ya makabila hutumia mbuzi katika shughuli za jamii kama mahari, vifo na sherehe za kimila
- Mbuzi huchukua muda mfupi kufikia umri wa kuuzwa au kuchinjwa ikilinganishwa na ng'ombe
- Matumizi ya nyama ya mbuzi anapochinjwa yanalingana na mahitaji ya familia bila ulazima wa kuhifadhi kwenye jokofu
- Hakuna pingamizi la kimila au kidini kuhusu ulaji wa nyama ya mbuzi ikilinganishwa na nguruwe

**Je, hali halisi ya ufugaji wa mbuzi Tanzania ikoje?**

Tanzania ina mbuzi zaidi ya milioni 24.5 (Jedwali namba 1) ambao hupatikana karibu katika kila kijiji. Pamoja na idadi hii, kipato kutokana na wanyama hawa bado ni kidogo. Hii inatokana na utunzaji usio wa kitaalam. Kufuatia hali hii, uzalishaji upo katika viwango vya chini kama inavyoonyesha katika mifano ifuatayo hapa chini:

i) Wanyama wa kienyeji hukua polepole (gramu 20-30 kwa siku)

ii) Vifo vya mbuzi hutokea mara kwa mara. Wakati mwingine vifo vya watoto hufikia hadi asilimia 50 na vile vya mbuzi wakubwa hufikia asilimia 30. Hii hali husababishwa na magonjwa ya mlipuko ya mapafu (CCPP- Contagious Caprine Pleuropneumonia, ambao una chanjo yake maalumu, hata wakachanjwa mara moja au mbili kwa mwaka inatosha), minyoo na lishe duni

iii) Mbuzi huchelewa kupata mimba kwa mara ya kwanza. Hii inatokana hasa na lishe hafifu

iv) Kuna muda mrefu kati ya mzao mmoja hadi mwingine

v) Uzito wakati wa kuzaa au kuchinja huwa ni mdogo na huchukua muda mrefu kufikia uzito huo

vi) Ubora wa nyama ya mbuzi hauridhishi kwa mahitaji ya soko

**Je ni mambo gani yanayochangia hali hii?**

i) Lishe hafifu

ii) Magonjwa

iii) Utunzaji mbaya

iv) Uduni wa wanyama bora hapa nchini na utumiaji mbaya wa madume

v) Kutokuwa na miongozo ya ufugaji bora wa mbuzi

**Uzalishaji utakuwaje kama ufugaji bora ukizingatiwa?**

i) Ukuaji wa mbuzi unaweza kuongezeka kutoka gramu 20 - 30 kwa siku hadi kufikia gramu 100 au zaidi kwa siku. Kwa hiyo, wanaweza kuuzwa wakiwa na umri wa mwaka mmoja baada ya kuzaliwa
ii) Vifo vinaweza kupungua hadi kufikia asilimia 10, kiwango ambacho kinakubalika
iii) Mimba ya kwanza inaweza kushika kati ya umri wa miezi 8 hadi 12 badala ya miezi 18 – 24. Ila inashauriwa anzia miezi 10 ili majike hayo yasidumae
iv) Kuongezeka kwa uzito wa mbuzi wakati wa kuuza au kuchinja
v) Kupatikana kwa nyama inayokubalika zaidi na hivyo kujipatia soko la uhakika hasa kwenye mahoteli na nje ya nchi (hasa Uarabuni)
vi) Mbuzi wanaweza kuzaa mara tatu katika miaka miwili

**Jedwali Na. 1**

| - AINA YA MBUZI | | |
|---|---|---|
| Small East African (SEA) | Gogo (3,867,319), Luguru (nk), Maasai (3,865,783), Newala (936,464), Pare white (2,933,391), Sonjo red (954,928), Sukuma (5,723,247) and Ujiji (2,906,855). | 19,188,987 |
| Anglo-Nubian & French Alpine | | 672 |
| Boers & Kalahari | | 2680 |
| Somalia (Isiolo) | | 785 |
| Malya (Blended) | | 1984 |
| Norwegian | | 2,216 |
| Saanen | | 1280 |
| Toggenburg | | 3459 |
| Chotara | | 2,001,735 |
| | Jumla kuu | 24,500,000 |

# SURA YA PILI

## UZALISHAJI

**Kuna aina ngapi za mbuzi?**

***Kuna aina (breeds) nyingi sana za mbuzi duniani (zaidi ya 300);*** **wa [illegible] a kumi nchini Tanzania, ambao ni"- Small East African-SEA ;(mbuzi wenye umb [illegible] balimbali (picha hapo chini inaonyesha dhahiri);. Malya, Boer, Kalahari, Galla, (Ang [illegible] Norwegian, Saanen, Toggenburg, makabila haya Galla, ni mbuzi wa maziw [illegible] ake).**

**Aina za mbuzi hutofautiana kwa ukubwa, umbile na wingi na [illegible] wa manyoya. Pia hutofautiana katika ukubwa na maumbile ya pembe zao, na masikio. [illegible] ya tofauti hizi nyingi. pia kuna njia nzuri sana kutumia madume makubwa kwa mbuzi majike [illegible] kienyeji ili kuongeza wingi wa nyama na ubora wake. Mfano mzuri ni madume ya kutoka Afrika ya kusini aina ya Boer na Kalahari kama picha zinavyoonyesha hapo chini.**



**A.Aina ya mbuzi wa Afrika ya Mashariki(SEA)**



**B.Aina ya mbuzi wa Afrika kusini, Boer**



**C.Dume la kisasa (Kalahari red, kutoka Africa ya kusini)**



**D.Dume la lisasa (Boer kutoka Afrika ya kusini)**



E Mbuzi hupenda kukwea miti (Browsers)

**Upatikanaji wa haya madume**

Haya madume yanapatikana kwenye shamba la mwekezaji mmoja Ubena Estate Farm, Morogoro. Ni rahisi kuwatumia hawa madume kuzaliana na mbuzi wa kienyeji. Utafiti umeonyesha matokeo mazuri sana. Vitoto vinavyozaliwa kutokana na hizi mbegu huwa na nyama nyingi na kuuzwa sokoni kwa bei nzuri kuliko wa kienyeji wenye nyama kidogo. Pia madume ya Somali yanapatikana Arusha.

**Kuna aina gani muhimu za mbuzi Tanzania?**

Nchini Tanzania kuna aina nyingi za mbuzi karibia sawa na makabila ya watu nchini:-

a) **Mbuzi wa kienyeji**
   - Gogo, Ujiji, Newala, Mbuzi weupe wa Kipare (Pare white), Shinyanga/Sukuma, Maasai, Sonjo, n.k.

b) **Mbuzi wa nyama walioboreshwa**
   - Boar na Kalahari kutoka Afrika ya kusini

c) **Machotara wa Mbuzi ya kisasa na wa kienyeji kwa nyama**
   - Ni mbuzi wanaofugwa sana na makabila mbali mbali Tanzania
   - Wengine huwa wadogo na wakubwa kutokana na mchanganyo wa hizo damu za mbuzi za aina nyingi ikiwa ni wa nyama na wa maziwa pia



**F. Mbuzi wa kienyeji (SEA)**



**G. Mbuzi wa Somali**

**Mbuzi wa Somali**

- Ni mbuzi wenye shingo zilizonyoka na vichwa vina rangi [illegible] sehemu nyingine za mwili na miguu zina rangi moja aidha nyeupe [illegible]. Mikia yao ni mifupi iliyonyanyukia juu. Hutunzwa sana kwa ajili ya [illegible]
- Mbuzi waliokomaa wana uzito mkubwa zaidi ya mbuzi [illegible] miguu mirefu na miembamba na kwato zao ni rahisi kupata ugon[illegible] sehemu zenye unyevunyevu. Ni mbuzi wanoaweza kuishi kwenye [illegible] ukame. Wana masikio madogo na pembe fupi.
- Mbuzi wa Somali hawatofautiani sana na mbuzi wa SEA, il[illegible] maumbile makubwa zaidi na wana nyama nyingi na ukuaji wao ni wa [illegible] zaidi.

**Kumbuka: mbuzi wa Boer na Kalahari ndio wanaopendekezwa katika kuzalisha machotara ya mbuzi wa nyama Tanzania. Hii ni kwa sababu machotara hao wanachukua muda mfupi kufikia uzito wa kuuza au kuchinjwa.**

## Upandishaji

**Je, utawapandisha mbuzi majike wakati gani?**

- Majike wadogo huanza kutoa mayai katika tumbo la uzazi wakiwa na umri wa miezi kati ya 6 na 8. Hata hivyo, inapendekezwa asipandishwe wakati huu.
- Inashauriwa apandishwe kwa mara ya kwanza akiwa na umri wa miezi 8 hadi 12 kutegemeana na ukuaji wake na umbile lake. Umbile lake linatakiwa liwe kubwa kumuwezesha kubeba mimba vizuri na kuzaa bila matatizo.
- Mimba ya mbuzi huchukua siku 150 au miezi 5. Baada ya kuzaa, mbuzi jike huja kwenye joto wiki 2 hadi 3 zifuatazo, lakini kuna mbuzi wengine hawapati joto mwezi mmoja mpaka miwili baada ya kuzaa kwa sababu ya kunyonyesha.
- Joto ni hali ya mnyama (mbuzi jike) kuhitaji dume kumpanda apate mimba.
- Joto la mbuzi hurudia kila baada ya siku 15 hadi 19 na muda wa joto ni saa 18 mpaka 24. Ni muhimu kumpandisha mbuzi jike mara anapoonekana yupo kwenye joto. Inabidi kutunza kumbukumbu za upandishaji, ili kuweza kufuatilia joto la mbuzi kwa nia ya kuelewa kama amepata mimba au la. Mbuzi akipandishwa miezi 3-4 baada ya kuzaa anaweza kuzaa mara 3 katika miaka 2 (Kwa kitaalam huu ndio mpango mzuri kumwezesha mbuzi jike kuwa na afya bora).

**Madume**

**Ni lini madume ya mbuzi yaanze kutumika?**

- Madume madogo huanza kutoa mbegu yakiwa na umri wa miezi 5 hadi 10. Lakini madume yaliyochaguliwa kwa jili ya uzazi yaanze kutumika kupanda majike machache yakifikia umri wa miezi kati ya 12 na 18. Baada ya umri wa miaka miwili, dume mmoja linaweza kukaa na majike kati ya 20 hadi 30 muda wote.

- Madume bora tu yatumike katika uzalishaji, mengine yahasiwe yakiwa na umri wa miezi mitatu na kukuzwa kwa nyama wafikapo miezi anzia 5 hadi miezi 8 ndipo wauzwe.

**Uchaguzi wa dume bora unazingatia sifa zipi?**

- Awe ametokana na wazazi wenye sifa nzuri za ukuaji (vinasaba vyenye rekodi nzuri), kuzaana na ubora wa maumbile.
- Ukuaji uwe mzuri sana ukilinganisha na madume mengine kundini.
- Awe na umbile kubwa na kujaza misuli sawasawa.
- Asiyeugua mara kwa mara.
- Awe na umbile la kiume na sehemu zake za uzazi ziwe sawasawa

**Kuzaliana kiukoo**

**Kuzaliana kiukoo ni nini na madhara yake ni nini?**

- Katika jamii zote za wanyama, kuzaliana kiukoo hakuruhusiwi kabisa. Hii ina maana kwamba si vyema kumpandisha dume kwa mama yake, mbuzi jike kwa baba yake, au hata kuwapandisha watoto wa baba na mama mmoja. Huko ni kuzaliana kiukoo.
- Matokeo ya kuzaliana kiukoo ni kupata mbuzi vilema au wanaokufa wakiwa wachanga. Aidha, watoto hao huzaliwa wakiwa wadhaifu na hukua kwa matatizo sana.

**Utazuiaje mbuzi wako kuzaliana kiukoo?**

Ili kuzuia mbuzi wako kuzaliana kiukoo, zingatia yafuatayo: -

- Wahasi au wauze madume wote waliozaliwa shambani mara baada ya kuachishwa kunyonya.
- Kama unaweza kuwa mwangalifu na makini, tunza kumbukumbu za upandishaji kila mwaka na hatimaye ufuatilie uhusiano wa mbuzi wako ili usipandishe mbuzi ambao wana uhusiano wa karibu.
-

**Zingatia: Madume yatumikayo kupanda yasikae katika kundi la majike yako kwa zaidi ya mwaka mmoja na inashauriwa wafugaji wabadilishane madume baada ya muda huo.**

## Malengo katika uzalishaji wa mbuzi wa nyama

Katika kuzalisha nyama ya mbuzi, lengo ni kupata nyama nyingi kwa mwaka na yenye ubora ambao mlaji atakuwa tayari kununua. Kwa hiyo lengo la kwanza ni kuwafanya mbuzi wazaliane kwa wingi kila mwaka. Lishe na afya bora kwa majike ya mbuzi ni muhimu kufanikisha hili. Aidha madume bora yatumike. Watoto wakizaliwa wawe na vifo vichache sana na wakue upesi. Majike wawe wazuri wenye maziwa ya kutosha ya kuwanyonyesha watoto wao na kufikia uzito mzuri wakati wa kuacha kunyonya. Baada ya kuacha kunyonya mbuzi wadogo wakue upesi na kujaza nyama (sio mafuta) nyingi katika miili yao. Mbuzi

wakubwa wana nyama nyingi zaidi. Hivyo basi tunahitaji mbuzi wenye uzito mkubwa na umbile kubwa. Ukiwa unauza mbuzi hai, mnunuzi aweze kupendezewa na ukubwa na umbile zuri la mbuzi wako; atanunua kwa bei nzuri. Wakati wa kuchinja na k[illegible] nyama ya mbuzi laini (tender), yenye mafuta kidogo lakini yenye nyama (le[illegible]) ili mlaji aweze kutupatia fedha nyingi.

## Kunenepesha mbuzi wa nyama

Mbuzi wetu wa kienyeji huchinjwa wakiwa na kilo 20 hadi 25 na huw[illegible] uzito huu baada ya miaka mitatu hadi minne. Hii inatokana na ukuaji hafifu wa gramu 15 hadi 25 kwa siku. Uzoefu toka sehemu nyingi zimeonyesha uwezekano wa kufupisha muda wa mbuzi kufikia uzito wa kuuza na kuboresha nyama yake kwa kuwanenepesha kwa kipindi fulani kabla ya kuchinjwa. Mbuzi wanaweza kunenepeshwa kwa kutumia masalio ya nafaka na mashudu.

**Kwa nini kunenepesha mbuzi ?** Kuna faida zifuatazo za kunenepesha mbuzi:

i) Wanakua kwa haraka zaidi na hivyo kuchinjwa wakiwa na uzito mkubwa zaidi
ii) Wanatumia vyakula vizuri zaidi; ina maana hutumia chakula kidogo kwa ongezeko la kila kilo ya uzito
iii) Wanafikia uzito wa kuchinja kwa muda mfupi na hivyo kufanya nyama yake kuwa laini zaidi
iv) Nyama inakuwa na mafuta ya kutosha; ndivyo wapendavyo wa-Tanzania wengi
v) Bei ya nyama kwa kilo inaongezeka tokana na mwonekano unaovutia
vi) Kutokana na ukuaji wa haraka, mbuzi wanaouzwa na mfugaji kwa mwaka huongezeka na hivyo kumwongezea kipato
vii) Ufugaji unakua wa kibiashara na kitaalam zaidi

### Jinsi ya kunenepesha

- Nunua mbuzi wenye afya nzuri na uzito wa kilo 14 hadi 18
- Wapumzishe kwenye uzio mbali kidogo na banda kwa siku 14 na wachunguze afya zao.Mbuzi wengi wana minyoo, kwa hiyo ni muhimu kuwapa dawa ya kuondoa minyoo na dawa za magonjwa mengine kama wanayo.
- Walishe ndani ya banda. Wape majani ya kutosha. Mbuzi aliyezoea kula majani tu anahitaji wiki tatu kuzoea chakula cha unenepeshaji.
- Walishe mchanganyiko ufuatao:
  - Pumba ya mahindi 70%
  - Mashudu ya alizeti au pamba 28%
  - Madini 2%

Walishe gramu 300 - 400 kwa siku. Kiasi cha protini kwenye chakula kisiwe chini ya asilimia 16. Mbuzi wawe na maji muda wote.Wanenepeshe mbuzi wako kwa muda wa miezi mitatu.Baada ya hapo ukuaji hupungua na wataanza kuweka mafuta mengi kwenye

nyama hali itakayowafanya wanunuzi wasiipende nyama hiyo. Aidha, gharama za ulishaji itakuwa kubwa.

... mahimu ya kuzingatia katika unenepeshaji ili kupata faida:

Hakikisha mbuzi wanatoka shambani mwako au umewanunua mbuzi wazuri kwa bei ya chini

Hakikisha kunakuwepo na chakula na maji kwenye banda muda wote. Wanyama wavivu kula chakula cha kunenepesha waondolewe kwenye unenepeshaji mara moja, watapunguza uzito. Kusiwe na msongamano kwenye banda.

c) Mbuzi wauzwe mara wanapofikia unene wa kutosha.

d) Ni vyema kutumia madume ya mbuzi yaliyohasiwa kwani huweka mafuta kwenye nyama mapema na nyama yake haina harufu ya beberu.

Chakula cha unenepeshaji kisiwe ghali. Aidha, nenepesha tu endapo bei ya kilo ya nyama toka kwa mbuzi aliyenenepeshwa itakuwa juu ya ile ya wasionenepeshwa. Tafuta soko la uhakika la nyama au mbuzi mjini ambako bei ya juu inaweza kupatikana.

# SURA YA TATU

# ULISHAJI

**Mbuzi hupenda kula nini?**

- Aina mbalimbali za majani; wanapochungwa huanza na yale laini. Mchanganyiko wa majani wanaokula mbuzi huwawezesha kupata viinilishe mbalimbali vya vyakula, kama vile protini, wanga (nguvu), madini na vitamin. Hii inawafanya wawe na afya nzuri na kukua kwa haraka.
- Matawi ya miti hasa mikunde kama vile lukina, mlonge, mfifi na migunga. Mbuzi hupenda kusimama na kula matawi ya miti tofauti na kondoo (angalia picha hadi wanakwea miti wakati wa ukame). Kwa hiyo, ni vyema mbuzi wachungwe kwenye maeneo yenye miti mifupi (bush) kwani watasimama na kuvuta majani na kuchagua yenye viinilishe vyote (hii husababisha nyama ya mbuzi kuwa tamu).



**H. Lukina (browsing)**



**I. Mbuzi hupenda kula juu Mfifi (*Gliricidia sepium*)**

- Mabua ya mahindi na mazao mengine kama nyasi za mpunga, maharage na ngano. (Mabua haya yanaweza kuboreshwa kwa kutumia mbolea ya urea, kinyesi cha kuku na majivu – hapa inahitajika elimu zaidi kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine au Afsa Ugani)
- Mabaki ya jikoni kama majani ya mboga (kabichi, mchicha na matembele) na maganda ya matunda mbalimbali
- Ngugu na hata Guatemala zinaliwa sana na mbuzi, ila zikatwe vipande vidogo vidogo kwa panga au mashine na kuwekwa kwenye vyombo maalum (*feed troughs*) kuzuia umwagikaji. Vyombo hivi vya chakula visafishwe kuzuia wadudu wanaoleta magonjwa ya kuharisha.
- Hakikisha mbuzi wanapata maji masafi ya kunywa baada ya kutoka machungani, sehemu maalumu ijengwe karibia na hori la kulia chakula (feed trough), nayo inaitwa hori la maji ya kunywa (water trough). Pawe pasafi wakati wote kuepuka mlipuko wa magonjwa.

**Ulishaji wa mbuzi**

**Kuna aina ngapi za ulishaji wa mbuzi?**

**Hapa Tanzania na mahali pengine katika nchi za joto kuna aina mbili kuu za ulishaji**

i. **Kuchunga**
ii. **Kuwalisha nyumbani**

**Kuchunga:**

**Huku ni kuwapeleka mbuzi machungani wazunguke wakila chochote wanachofanikiwa kukifikia au kuwafunga kwa kamba (tethering) hapa na pale porini (hasa kama ni kundi dogo). Inashauriwa kuwahamishia wanyama kwenye sehemu mpya zenye majani mabichi mara kwa mara ili kuwawezesha wapate viinilishe na virutubisho vya kutosha.**

- **Huu ni mfumo wa ufugaji wa mbuzi wa nyama unaotegemewa sana Tanzania. Hii ni kwa sababu, ukiwa na mbuzi wengine (50 au zaidi), ni vigumu kuwalisha ndani ya banda kwa muda wote. Pia kuchungia nje kunawapa mbuzi mazoezi na afya nzuri kuliko kuwafungia ndani muda wote. Ila usiku walale kwenye banda lao kwa ulinzi na usalama wao**
- **Muda wa mbuzi kuchungwa usipungue saa 8 kwa siku ili washibe na kupata viinilishe na virutubisho vya kutosha wanavyostahili kwa afya zao.**
- **Eneo la kuchungia liwiane na wingi wa wanyama ili wapate chakula cha kutosha na kuzuia uwezekano wa milipuko ya magonjwa, na mmomonyoko wa udongo.**
- **Mbuzi wasilishwe sehemu moja kila siku, bali wazunguke maeneo mbalimbali (Rotational grazing). Mzunguko huo pia hutoa nafasi kwa malisho kuota upya sehemu moja wakati mbuzi wamehamishiwa sehemu nyingine.**

**Faida za kuchunga**

- Gharama za ulishaji ni ndogo kwa sababu mnyama anajitafutia anachotaka
- Wanyama wanapata hewa ya kutosha, afya nzuri na kuchangamka zaidi kulingana na hali ya hewa hasa kama kuna jua la wastani na hakuna mvua.

**Kuwalisha nyumbani**

Mbuzi hufugwa kwenye banda, boma au kufungiwa kando ya banda. Chakula kama majani huletwa kwa mnyama (*Cut and carry*). Kwa kawaida mfumo huu wa ufugaji unafaa pale tu mfugaji akiwa na wanyama wachache na hana maeneo makubwa ya kuchungia.

**Faida za kulisha nyumbani**

- Mbuzi hawahitaji eneo kubwa la malisho
- Wanaweza kutumia mazao na mabaki mengi ya shamba kama vile majani ya migomba, mahindi, mabaki ya maharage na hata matawi ya miti mbalimbali (Lukina, mfifi, n.k)
- Inapunguza muda wa kuchunga. Wanaweza kuzungushiwa boma ili wapate mazoezi na sehemu ya kupata jua (Vitamini D)
- Ni rahisi kupanga na kumudu uzazi
- Huzuia mbuzi kuharibu mazao kwa majirani na kuepuka ugomvi nao
- Inarahisisha ukusanyaji wa mbolea
- Hupunguza maambukizi ya magonjwa, ila mbuzi wasisongamane kwenye banda

Hata hivyo, katika hali halisi ya wafugaji, si rahisi kuwalisha mbuzi nyumbani. Kwa kawaida mbuzi wa nyama ni wa kuchungwa na wa maziwa huchungiwa ndani kulinda kiwele na chuchu za maziwa zisikwaruzike na miiba au senyenge (barbed wire).

**Ni mambo gani ya kuzingatia katika ulishaji wa mbuzi?**

- Lisha chakula kisafi na majani yasiyo na unyevunyevu
- Maji na vyombo viwe visafi
- Mbuzi wapate mchanganyiko wa vyakula vyote yaani majani ya asili, nyasi, mikunde na madini
- Mbuzi wanaolishwa ndani wanaweza kuwekewa vitita vya majani wakati wote na kutundikwa kwa kamba ukutani
- Tumia mabaki ya mazao kama mabua ya mahindi, mtama na mabaki ya maharage, ngano, n.k. Ubora wa mabaki haya unaweza kuongezeka kama ukichanganya na mollasis, urea kutegemea na upatikanaji wake.
- Miezi miwili mpaka mitatu kabla ya kuuza mbuzi, mabaki haya na mashudu yanaweza kutumika kumnenepesha mbuzi ili apate bei nzuri wakati wa kuuza
- Mbuzi wa marika yote wapewe jiwe la kulamba (madini).

- Aina ya mikunde laini isilishwe kwa wingi kwa vile mbuzi huweza kuvimbiwa (bloat)
- Chakula kisiwekwe sakafuni. Hii ni kwa sababu kinaweza kuharibika na kuchafuliwa na vijidudu, kinyesi na mkojo.
- Ulishaji wa mbuzi kwenye mashamba ya mahindi, mtama, n.k. baada ya mavuno husaidia sana hasa wakati wa kiangazi. Vile vile rutuba ya udongo huongezeka kutokana na kinyesi cha mbuzi
- Utumiaji mzuri wa miti ya malisho huongeza lishe bora kwa mbuzi. Miti hii ni kama lukina, Mlonge, Sesbania, Mfifi, Migunga na Kaliandra. Inaweza ikaoteshwa mipakani mwa shamba la mazao au hata ndani ya shamba. Ikiwezekana mbuzi wapewe majani ya miti hiyo baada ya kutoka machungani
- Miti ya asili kama migunga, mikwaju, n.k. isikatwe ovyo ovyo sehemu wanakochungia mbuzi. Matunda na majani ya miti kama hiyo ikichanganywa na malisho huboresha chakula kwa kuongeza protini
- Majani ya asili yanaweza kuboreshwa kwa kusia mbegu za mikunde katika mbuga hizo za malisho
- Kutegemeana na hali ya uchumi, mbuzi huweza kupewa vyakula vya ziada kama pumba, mashudu na mchanganyiko wa madini (na hasa jiwe la kulamba)

# SURA YA NNE

# AFYA YA MBUZI

**Utangulizi**

Mbuzi wakishambuliwa na magonjwa huwa wanaonyesha dalili zinazomuashiria mfugaji kuwa mbuzi wanaumwa. Wafugaji wanashauriwa kutambua mapema dalili za mwanzoni kabisa. Dalili kubwa ni kujitokeza kwa hali isiyokuwa ya kawaida kwa mbuzi. Hivyo basi, ni muhimu kwa mfugaji awe na ufahamu mzuri na mbuzi wake na awe anawafuatilia kwa karibu ili aweze kugundua mabadiliko yoyote yasiyo ya kawaida yatakayotokea. Mara tu ugonjwa wowote utakaposhukiwa kujitokeza, mfugaji anapaswa kutoa taarifa kwa mganga wa mifugo mapema ili huduma ipatikane kwa haraka na kuzuia vifo.

Ni muhimu kuelewa hali ya afya ya kawaida kwanza ili baadaye uweze kutambua hali isiyo ya kawaida ambayo ni ya ugonjwa.

**Je ni madhara gani yatokanayo na mbuzi wasio na afya nzuri?**

Mbuzi wasio na afya nzuri humletea mfugaji hasara za kiuchumi kutokana na:-

- Vifo
- Kupungua uzito
- Kukua polepole na kuchelewa kufikia uzito wa kuuza
- Gharama kubwa za matibabu

- Baadhi ya magonjwa ya mbuzi huathiri binadamu (*Zoonotic*)
- Kutupa mimba

**Mbuzi mwenye afya anaonekanaje?**

- Amechangamka na kichwa chake huwa juu.
- Macho yake ni maangavu. Pia huzungusha masikio pindi inapotokea sauti.
- Mwili wake umejaa vizuri (hajakonda)
- Manyoya yanang'ara na yanalala vizuri juu ya ngozi yake.
- Anakutana na wenzake kwenye kundi.
- Anakula vizuri kisha baadaye anacheua na kutafuna tena (*chewing the cud*)
- Anatoa kinyesi kawaida
- Vipimo vya mwili ni vya kawaida (joto la mwili 38.5⁰C hadi 39⁰C) na mapigo ya moyo ni 70-80 kwa dakika, haraka zaidi kwa watoto
- Anavuta pumzi mara 22-26 kwa dakika moja, haraka zaidi kwa watoto
- Rangi ya ngozi ya ndani ya jicho ni ya rangi ya uwaridi (pink)

**Dalili gani zinazoonyeshwa na mbuzi waslo na afya nzuri?**

- Mbuzi kujitenga na wenzake
- Kuachia kichwa kiende chini
- Kupunguza hamu ya kula na hata kutokula kabisa
- Kutokuwa mchangamfu (kuzubaa)
- Kusisimuka manyoya, kuonekana hana nguvu, kuchoka na inzi hutua mwilini mwake
- Kuishiwa nguvu na kushindwa kusimama na kutembea
- Kubadilika kwa vipimo vya joto, mapigo ya moyo na kuvuta pumzi
- Kuharisha au kutoa kinyesi kigumu kupita kiasi
- Kupumua kwa shida

**Kumbuka: NI RAHISI KUZUIA KULIKO KUTIBU**

Kuzuia magonjwa hutumia fedha kidogo tu kulinganisha na gharama za kutibu ambazo ni pamoja na madawa ya bei kubwa, hasara kutokana na vifo, na kushuka kwa uzalishaji. Kwa hiyo hapa tumeorodhesha baadhi ya magonjwa muhimu ya mbuzi hapa Tanzania.

**Kuna makundi mangapi ya magonjwa ya mbuzi?**

Mbuzi, kama walivyo wanyama wengine wafugwao, huweza kushambuliwa na magonjwa mengi. Magonjwa haya yametapakaa na kuenea mikoa yote Tanzania na kuathiri kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa mbuzi. Magonjwa ya mbuzi yanaweza kupangwa katika makundi makuu yafuatayo:

a) Magonjwa yanayoambukizwa kwa haraka na yenye kutia hasara kubwa (magonjwa ya mlipuko) kama vile Homa ya Bonde la Ufa (*Rift Valley Fever*, RFV), ugonjwa wa miguu na midomo (FMD) na homa ya mapafu (CCPP)
b) Magonjwa yasiyo ya mlipuko lakini yanayoua mbuzi kwa wingi kwa mfano Kimeta
c) Magonjwa yanayoifanya Tanzania kutokubalika kuuza mifugo yake na mazao ya mifugo katika soko la kimataifa, k.m. FMD
d) Magonjwa yanayoambukiza wanadamu (Zoonoses), k.m. Kimeta, *Orf*, Homa ya bonde la Ufa (Rift Valley Fever - RFV)

## Minyoo

**Minyoo ni nini na inapatikana wapi?**

Minyoo ni viumbe hai wenye ukubwa mbalimbali ambao wanaishi kwa kutegemea wanyama wengine. Minyoo wanapatikana katika tumbo, utumbo, maini na mapafu ya wanyama.

**Dalili za Mbuzi wenye minyoo ni zipi?**

Mbuzi anaweza kuonyesha baadhi ya dalili zifuatazo:

- Vifo vya ghafla hasa kwa watoto wa mbuzi
- Hamu ya chakula inashuka, wanakuwa hawana nguvu na tumbo kuvimba
- Manyoya yaliyosimama na yasiyopendeza
- Kupungukiwa damu (Macho huwa meupe badala ya rangi ya pinki)
- Kuharisha
- Mbuzi hupunguza ukuaji na hukonda
- Mbuzi pia huwa wanashambuliwa na majipu na ORF (picha chini)
- Kuzuia usagaji wa chakula tumboni na wakati mwingine kuziba utumbo
- Mbuzi wakubwa huwa dhaifu na hatimaye hufa



J.Mbuzi mwenye jipu chini ya shingo



K.Mbuzi mwenye ugonjwa wa "ORF", vidonda



L.Mbuzi mwenye minyoo bila tiba (Dhaifu sana)



M. Mbuzi mwenye ugonjwa wa mapafu (CCPP

**Kutibu na kuzuia minyoo kwenye mbuzi**

- Tumia dawa ya kuua minyoo mfano: Albendazole (ya kunywesha/maji au vidonge), Levamisole (yakuchoma chini ya ngozi), Ivomectin (yakuchoma chini ya ngozi)
- Banda liwe safi pia nyunyizia dawa ya kuua wadudu
- Njia nyingine ya kuzuia magonjwa ni kupitia chanjo. Hapo juu kuna orodha ya baadhi ya magonjwa ya kawaida unayopaswa kuchanja katika hatua tofauti. Hakikisha unapata Mtaalamu wa mifugo kuchanja mbuzi wako. Usifanye mwenyewe.
- Tumia dawa za minyoo kila baada ya miezi mitatu hasa wakati wa masika.s

**Muhimu:** Tafuta ushauri wa wataalam (Daktari wa mifugo au Afisa ugani) kuhusu matumizi ya madawa.

## Ugonjwa wa kuharisha damu (*coccidiosis*)

**Ugonjwa wa kuharisha damu unasababishwa na nini?**

Ugonjwa wa kuharisha damu unaweza kusababishwa na vitu vingi, lakini mara nyingi huletwa na vimelea vinavyoitwa *coccidia*

- Mbuzi wadogo huathirika zaidi kutokana na chakula na maji yenye vimelea
- Vimelea hutoka kwenye kinyesi cha mbuzi wakubwa na kuchafua mazingira

**Dalili za ugonjwa wa kuharisha damu ni nini?**

- Kushindwa kula, kukosa nguvu na kukonda
- Kuharisha damu na kujikamua wakati wa kuharisha
- Vifo vya mbuzi wadogo

**Je unawezaje kuzuia na kutibu ugonjwa wa kuharisha damu?**

- Kutumia sulphadimidine na amprolium
- Tenganisha wagonjwa na kuwatibu
- Weka mbuzi sehemu safi na kavu
- Hakikisha kinyesi hakichafui maji na chakula
- Punguza msongamano wa mbuzi katika banda

## Ugonjwa wa moyo kujaa maji (*Heartwater*)

**Ugonjwa wa moyo kujaa maji ni nini?**

- Ugonjwa huu unaodhuru ng'ombe, mbuzi na mbuzi unaletwa na vimelea vinavyosambazwa na kupe

**Dalili za ugonjwa wa moyo kujaa maji ni zipi?**

- Homa kali na kupoteza hamu ya kula
- Dalili za kichaa kama kupoteza utaratibu wa hatua, kutembea kwenye mduara na kusaga meno
- Kuanguka, kutetemeka, kupiga mateke na halafu kufa
- Maji mengi kwenye moyo, kifua na tumboni mwa mzoga

**Je utazuiaje ugonjwa wa moyo kujaa maji?**

- Tumia dawa ya josho kuuwa kupe
- Tumia dawa ya tetracycline kutibu wagonjwa

## Kuoza kwato (*Foot rot*)

**Ugonjwa wa kuoza kwato ni nini?**

- Ugonjwa huu wa kuoza kwato unasababishwa na bakteria ambao huzaliana kwenye kwato
- Maambukizi hutokea kwenye matope hasa kipindi cha mvua

**Dalili za kuoza kwato ni zipi?**

- Kuvimba miguu na kwato kuwa na joto
- Vidonda kwenye kwato vinavyosababisha maumivu makali
- Kuchechemea

**Je, unazuiaje na kutibu ugonjwa wa kuoza kwato?**

- Weka mbuzi sehemu kavu
- Kata kwato ndefu
- Tibu vidonda kwa kuviosha na kuweka dawa
- Tumia dawa ya sindano ***sulphadimidine*** kutibu

## Homa ya Bonde la Ufa (*Rift Valley Fever*)

**Ugonjwa wa homa ya Bonde la Ufa ni nini?**

- Ni ugonjwa wa mlipuko unaosababishwa na virusi na kusambazwa na mbu
- Unaathiri mbuzi, kondoo, ng'ombe na binadamu

**Dalili za homa ya Bonde la Ufa ni zipi?**

- Homa
- Kutokwa na makamasi
- Kutupa mimba
- Vifo vya mbuzi wadogo

**Je, unazuiaje na kutibu ugonjwa wa homa ya bonde la ufa?**

- Chanja mbuzi
- Kuzuia mazalia ya mbu

## Ugonjwa wa miguu na midomo (*Foot and Mouth Disease* - FMD)

**Ugonjwa wa miguu na midomo ni nini?**

- Ni ugonjwa wa mlipuko unaoathiri mbuzi, kondoo, nguruwe, ng'ombe na wanyama pori unaosababishwa na virusi

**Dalili za ugonjwa wa miguu na Midomo ni zipi?**

- Homa kali
- Kutokula
- Vivimbe au vidonda kwenye ulimi, fizi, midomo, puani, miguuni, kwenye chuchu na kiwele
- Kuchechemea na kutokwa mate mengi mdomoni

**Je utazuiaje ugonjwa wa miguu na midomo?**

- Karantini ya kuzuia usafirishaji wa mifugo na mazao ya mifugo
- Chanja mifugo kila mwaka au kila mlipuko utokeapo.

## Magonjwa ya mapafu (*Pneumonia*) na CCPP (Contagious Caprine Pleuropnemonia)

**Ugonjwa wa mapafu ni nini?**

- Ni ugonjwa unaoathiri mapafu ya mbuzi unaosababishwa na vimelea vya aina nyingi kama virusi, bakteria, *mycoplasma*, *chlamydia* na minyoo ya mapafu

- Huu ugonjwa CCPP kwa mbuzi pekee (kondoo hapana) huwa unajionyesha kama pneumonia na tofauti ni ndogo ila huwa unaua mbuzi wengi kwa pamoja. CCPP ina chanjo kama ilivyosemwa hapo awali

**Dalili ya ugonjwa wa mapafu ni zipi?**

- Kukohoa
- Kutokwa makamasi
- Kupumua kwa shida
- Vifo

**Utazuiaje ugonjwa wa mapafu?**

- Weka mbuzi sehemu safi na kavu
- Epuka msongamano wa mbuzi

## Kimeta (Anthrax)

**Ugonjwa wa kimeta ni nini?**

- Ni ugonjwa hatari unaoathiri wanyama wote wenye damu moto pamoja na binadamu unaosababishwa na bakteria

**Dalili za kimeta ni zipi?**

- Homa kali
- Vifo vya ghafla bila dalili nyingine
- Kupumua kwa shida
- Kutetemeka na kifafa
- Kusitisha kucheua
- Kutupa mimba
- Kutoka damu nyeusi isiyoganda kwenye matundu ya mwili
- Mzoga wa kimeta hauonyeshi kugangamala misuli

**Utazuiaje ugonjwa wa kimeta?**

- Chanja mifugo
- Karantini ya usafirishaji wa mifugo
- Mzoga wa kimeta umwagiwe chokaa na ufukiwe au uchomwe moto bila kupasuliwa

Mfugaji anapoona dalili za ugonjwa huu kwenye mbuzi anashauriwa kumwona daktari wa mifugo ili aweze kuutambua ugonjwa na kutibu. Aidha, mfugaji atapewa ushauri wa njia sahihi za kukinga wanyama wake wasiambukizwe na kuugua tena hapo baadaye

## SURA YA TANO

## MABANDA

**Hali halisi ya mabanda ya mbuzi Tanzania**

Mbuzi huchungwa porini pamoja na ng'ombe na kondoo. Wakirudi jioni huwa wanawekwa kwenye boma lililozungushiwa aidha kwa miiba, ukuta wa miti au mabanzi. Wakati mwingine huishi nyumba moja na wanaadamu. Kwenye maboma, mbuzi hunyeshewa mvua na mara nyingi hukaa kwenye mazingira ya matope. Matatizo mengi yanaambatana na ufugaji wa namna hii, ikiwa ni pamoja na kuingiliwa na wanyama wakali, uchafuzi wa mazingira, maambukizi ya magonjwa hata kwa wanaadamu (Zoonosis).



N. Banda la juu la mbuzi



O. Ndoo ya plastic ya kunywea maji masafi

**Je, ni muhimu kujenga banda la mbuzi?**

Umuhimu mkubwa wa banda kwa wanyama hawa, kama ilivyo kwa wanyama wengine wowote ni katika kuwapa kivuli, kuwakinga na mvua na wanyama wa porini na kuzuia wezi. Katika ufugaji wa kisasa wa mbuzi, banda linajengwa ili kukidhi mambo mawili:

a) Kuyaweka mazingira ya mbuzi katika ubora zaidi
b) Kurahisisha huduma kwa mbuzi (kulisha, kutibu, kuchanja n.k.)

Mbuzi huhitaji mazingira ambayo: -

a) Sio baridi wala joto sana
b) Yasiyo na unyevunyevu wala matope
c) Yasiyo na wadudu kama vile inzi, viroboto, utitiri, n.k.
d) Yenye hewa safi, mwanga na nafasi ya kutosha
e) Sehemu nzuri ya kulia chakula pamoja na maji



P. Hori la kulia chakula

**Aina gani ya banda hufaa kwa ajili ya mbuzi?**

Aina ya banda la mbuzi hutegemea mfumo wa ufugaji pamoja na idadi ya mbuzi wanaofugwa:

a) Banda la gharama huweza kuhitajika pale tu ambapo uzalishaji ni wa kiwango cha juu. Ni lazima kulinganisha kipato na gharama za banda.

b) Katika ufugaji wa kuwachunga mbuzi katika nyanda za malisho (porini), banda la kawaida linatosha. Banda kama hilo linaweza kuwa na paa, au likawa la kuweka mbuzi sehemu moja wakati wa usiku

**Ni vifaa gani vitumike kujenga banda la mbuzi?**

Inasisitizwa kwamba vifaa vya kujengea banda la mbuzi viwe ni vile vinavyokidhi haja bila kuwa na gharama sana. Pia viwe ni vile vinavyopatikana kwa urahisi katika eneo la mfugaji:

i. **Paa**
- Katika nchi za joto kama Tanzania, paa ni muhimu katika nyumba ya mbuzi kwani humsitiri mbuzi kutokana na jua kali na mvua
- Ni vizuri paa likawa na mteremko wa kutosha ili liweze kuhimili upepo mkali na kupunguza uwezekano wa kuvuja
- Vifaa vitumikavyo kuezekea banda ni nyasi, makuti ya minazi, makuti ya michikichi, majani makavu ya migomba, vigae na bati

ii. **Kuta**

Kuta za banda la mbuzi mara nyingi hupashwa kutoa fursa ya hewa kuzunguka nje na ndani ya banda. Hali hiyo ni muhimu katika,
- Kuondoa joto na kupunguza unyevunyevu
- Kuondoa hewa chafu toka bandani na kuingiza hewa safi
- Wakati mwingine ukuta huweza kuzibwa sehemu fulani kulingana na kinachopashwa kuzuiwa kisiwafikie mbuzi kama vile upepo mkali. Palipo na wasiwasi wa wanyama wakali na/au wizi, ukuta sharti uwe imara

Vifaa vinavyoweza kutumika kwenye kuta ni nguzo, fito, mabanzi, udongo, bati, waya meshi na matofali.

iii. **Sakafu**

Kinachohitakiwa katika utengenezaji wa banda la mbuzi ni sakafu kuwa kavu wakati wote. Ingawa ni vizuri kuwa na sakafu iliyoinuliwa kufanikisha suala la ukavu. siyo lazima sana kuinua sakafu kwani sakafu ya chini inaweza kuwa na mteremko unaoweza kutiririsha maji na mkojo kutoka kwenye banda

Vifaa vinavyoweza kutumika kwenye matengenezo ya sakafu ya chini ni mbao, miano, mabanzi, fito na wayameshi imara.

## SURA YA SITA

## UTUNZAJI KUMBUKUMBU

**Je, kumbukumbu ni nini?**

Kumbukumbu ya mbuzi ni kuweka kwenye maandishi idadi ya mbuzi mfugaji alio nao. jinsi ya kuendeleza uzao, kuwatibia, kuuza nyama, mbolea, na kuwauza mbuzi wazima kwa tija. ili iwe ni kwa biashara iletayo faida kwa mfugaji. Kama vitega uchumi vingine, utunzaji wa kumbukumbu ni muhimu sana ili kujua ufanisi wake hasa mapato na matumizi. Kumbukumbu husaidia kufuatilia maendeleo ya kila mbuzi, hutuwezesha kuelewa mbuzi wazuri na wabaya. Pia kumbukumbu hutumika kutathimini magonjwa na matatizo mengine yaliyopo katika kundi lako la mbuzi. Waghani watakushauri vizuri zaidi wakiziona kumbukumbu zako.

**Utunzaji wa kumbukumbu za mifugo**

Kuweka kumbukumbu za mifugo ni muhimu katika uzalishaji kwa ajili ya kutambua kosaafu. gharama za utunzaji na faida. Pia, humsadia mfugaji kufanya maamuzi katika uendelezaji wa ufugaji wake. Mtalaam wa mifugo pia anaweza kutumia kumbukumbu hizi ili kumsaidia mfugaji kuboresha ufugaji wake.

**Kuna aina ngapi za kumbukumbu?**

- Kuna aina nyingi za kumbukumbu kutegemeana na mfugaji anataka kufuatilia kitu gani kwa mfano mapato na matumizi, maendeleo ya kila mbuzi. Jinsi ya kuandika kumbukumbu hutofautina pia. Wengine hufuata majedwali maalumu yaliyoandaliwa na wataalam wa mifugo na wengine huandika wapendavyo wenyewe. Hapa tunapendekeza aina chache za kumbukumbu unazoweza kuandika:

i) Kumbukumbu za uzazi: Onyesha mbuzi gani amezaa, lini, jinsia ya mtoto, baba wa mtoto, aina (breed) na ikiwezekana uzito wa kuzaliwa

**Jedwali na. 2**

| Tarehe ya kuzaliwa | Na. ya mbuzi | Jinsia | Aina | Namba ya | | Uzito wa kuzaliwa (kilo) | Mengineyo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Baba | Mama | | |
| | | | | | | | |

ii) Kumbukumbu za chanjo na matibabu: Andika tarehe ya tukio, namba ya mbuzi, aina ya chanjo/ugonjwa aliokuwa nao, aina ya dawa iliyotumika na gharama za matibabu

iii) Kumbukumbu za ukuaji: Kama mbuzi wanapimwa uzito mara kwa mara, ni muhimu kuweka kumbukumbu za huo uzito. Inafaa kuandika tarehe ya kupima, namba ya mbuzi na uzito wake. Ongezeko la uzito linaonekana vizuri zaidi ikiwa, uzito wa mbuzi mmoja utapangwa katika mstari mmoja.

**Jedwali na. 3**

| Na. ya mbuzi/jina | Tarehe ya kupima uzito (kilo) | | | | | | Mengineyo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.11.2020 | 15.3.2020 | | | | | |
| Ishia/157 | 10.5 | 14.6 | | | | | |

iv) Kumbukumbu nyinginezo: Kama tulivyosema hapo juu, unaweza kuandika mambo mengine yanaohusu mbuzi wako kwa mfano, kuachisha kunyonya, kuuza mbuzi, kuhasi mbuzi, manunuzi mbalimbali (dawa, vifaa, vyakula). Ni muhimu kuandika tarehe ya tukio.

**Utawezaje kuwatofautisha mbuzi kabla ya kutunza kumbukumbu?**

Ili mfugaji aweze kutunza kumbukumbu za kila mbuzi, inabidi aweze kuwatofautisha kwa kuwapa vitambulisho. Njia zifuatazo zinaweza kutumika: -

a. Kwa kuwavalisha kamba zenye vibao vyenye namba shingoni
b. Kuwapa majina, kwa mfano Sabasaba, Ufunuo na kadhalika
c. Kuwaweka hereni (ear-tag) za plastiki au za chuma kwenye masikio